

Isaya 34:11 “KAATI na NUNGU wataimiliki, bundi na kunguru watakaa huko, naye atanyosha juu yake kamba ya ukiwa na timazi ya utupu”.

Jibu: “Kaati” ni “bundi wa jangwani” (*wanaoishi majangwani*), na chakula chao ni jamii za panya na wadudu..*Tazama picha chini.*



“Nungu” ni aina nyingine ya bundi wanaopatikana katika misitu yenye miti iliyozeeka, yenye matundu. Aina hii ya bundi hutoa mlio mkali wakati wa usiku wanapowasiliana na jamii zao, na ndio wanaosikika katikati ya jamii za watu (*Tazama picha na video chini*).



Lakini swali ni je? Bundi hawa (*Kaati na Nungu*) ni roho za

kichawi/majini?.

Jibu ni la!.. Bundi ni ndege tu kama ndege wengine walioumbwa na Bwana **MUNGU**, kama wakiwa katika mazingira yao ya asili, ni ndege tu kama ndege wengine, wanaohitaji pia kutunzwa.

Lakini pia ndege hawa wanaweza kutumika na wachawi katika shughuli za kichawi, kama tu vile kuku anavyoweza kutumiwa katika kafara za kichawi, na bundi ni hivyo hivyo, ila kwa mtu aliyeokoka hakuna silaha yoyote yenye uhai, au isiyo na uhai itampata.

Lakini kwa mtu aliye nje ya KRISTO, basi ni haki yake kuogopa bundi, na viumbe wengine kwani ni kweli yupo hatarini kudhuriwa na ibilisi.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge

na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Nimekuwa kama mwari nyuni wa jangwani,

IVUMBUE INJILI YA KRISTO KUTOKA KATIKA KILA JAMBO.

Je! Ni dhambi kumpiga au kumuua mnyama bila sababu yoyote?

Mjombakaka ni nani kwenye maandiko? (Walawi 11:29)

Hawa ndege katika Walawi 11:13-19 ndio ndege gani kwasasa?

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp